**Learning by Ear 2011/2012 – Corruption – The Elephant in the Room**

**Episode 05 – "Can They 'Stop Corruption Now'?"**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

- NARRATOR

Scene 1:

- Jeffrey (MALE, 58)
- Journalist 1 (FEMALE, 30)
- Journalist 2 (MALE, 30)
- Journalist 3 (FEMALE, 25)
- 2-3 more journalists

Scene 2:

- Jeffrey (MALE, 58)
- Sylvia (FEMALE, 19)
- NARRATOR

Scene 3

- Isaac (MALE, 22)
- Peter (MALE, 25)

**Intro:**

**0. Narrator:**

Hujambo na karibu katika sehemu hii ya tano kwenye mfululizo wa vipindi vya Learning By Ear, “**Noa Bongo Jenga Maisha yako**” tukiwa bado kwenye ile hadithi kusuhu suala la ufisadi kwa jina “**Tembo Nyumbani**”. Katika kipindi kilichotangulia, wabunge wanaohusika na kashfa ya ufisadi katika sekta ya nishati wanakutana kupanga mikakati ya kufadhili kampeni za uchaguzi. Wanapanga kuongeza kima cha fedha wanazopata kutokana na kandarasi bandia ili kufanikisha kampeni za mmoja wao John Maina, anayegombea kiti cha urais kuingia Ikulu. Walitarajia kwamba mfanyabiashara mashuhuru, Alfayo Odhiambo, ambaye ndiye mwanakandarasi mashuhuri katika njama yao, atafurahi kusikia kiwango cha biashara kinachoongezwa na kuendelea kuwauzia mita za umeme kupitia kashfa hii, lakini kwa mshangao mfanyabiashara huyu anakataa katakata kushirikiana nao. Badala yake anapanga njama ya kufichua kashfa hiyo, na ameamua liwe liwalo atajitokeza hadharani. Kwa upande wake, John Maina, bado anaongoza katika mkumbo wa wagombeaji urais. Kupitia mahojiano ya televisheni mgombea huyu, John Maina, anatangaza hatua kali zaidi za kuangamiza kabisa ufisadi.

Katika kipindi cha leo, "**Je unanaweza kukomesha ufisadi**?" Familia ya Odhiambo, ikishirikiana na rafiki yao wa karibu Jeffrey Thiongo, imezindua shirika jipya la kukabiliana na ufisadi. Na tunaungana naye katika mkutano na waandishi wa habari.

**<u>Scene One:</u>**

**1. SFX:** **Press conference, Photo cameras clicking**

**2. Jeffrey:** Hamjambo mabibi na mabwana, waandishi wa habari. Nashurukuru sana kwa kufika kwenu na kuendelea kuniunga mkono. Huu ni mkutano wa kwanza kuandaliwa na shirika letu, "**Komesha Ufisadi Sasa**" Na Kama mjuavyo, kazi iliyoko mbele yetu ni kubwa katika kupambana na ufisadi nchini mwetu. Kwa upande wetu tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba azma hii inatimia. Lakini nitaanza kwa kujibu maswali yenu.

**3. Journalist 1:** Bwana Thiongo, tunafahamu kwamba wewe umefutwa kazi katika halmashauri ya kupambana na ufisadi, tueleze ni kwanini?

**4. Jeffrey:** Ndio, Haya yalitokea baada ya kufahamu kwamba nyingi ya kesi nilizokuwa nikizifuatilia au kuzifanyia uchunguzi, zilikuwa zikizimwa. Na hata mara nyingine faili za kesi hizo kutoweka kabisa katika mazingira ya kutatanisha.

**5. Journalist 1:** Unamaanisha zimekuwa zikipotea?

**6. Jeffrey:** Hasa! Na kisha baadaye niligundua kashfa kubwa inayoendelea katika sekta ya nishati. Kwamba kampuni nyingi bandia zimefunguliwa na kupewa kandarasi ya kusambaza umeme kwa taifa. Lakini cha kushangaza licha ya kulipwa mabilioni ya pesa, kampuni hizi zote ni bandia.

**9. Journalist 3:** Na kwanini hatujasikia kuhusu kashfa hii?

**10. Jeffrey:** Kwasababu mwenyekiti wa halmashauri ya kupambana na ufisadi nchini, anafanya kila juhudi kuhakikisha kuwa kesi hizi zinazimwa. Wakati nilipojaribu kuhoji kesi hii ifufuliwe na kuchunguzwa upya, alinitisha kuwa utendaji kazi wangu hauridhishi na ndio ikawa sababu kubwa ya mimi kuachishwa kazi.

**11. Journalist 3:** Kwayo unamaanisha mwenyekiti wa halmashauri hii, pia ni mshirika katika kashfa hii?

**12. Jeffery:** Bila shaka anahusika pakubwa.

**13. Journalist 2:** Nani mwengine anahusika?

**14. Jeffrey:** Kashfa hii inahusisha maofisa wa ngazi za juu zaidi katika wizara ya nishati. Lazima kuna wabunge kadhaa wanaohusika na sakata hii, la sivyo haingeweza kuendelea kufika pale ilipofika sasa. Na pia wasiwasi wangu ni kwamba huenda kashfa hii ikaongezeka hata zaidi hasa wakati huu tunapokaribia kufanya uchaguzi mkuu.

**15. Journalist 1:** Madai haya ni mazito sana! Je! Una ushahidi wowote?

**16. Jeffrey:** Ushahidi upo! Nina stakabadhi za kuthibitisha madai haya baada ya uchunguzi wa kina niliofanya. Na nitawapa nakala za ushahidi huo baada ya huu mkutano.

***KW Anfang***

**17. Journalist 2:** Mbali na sakata hil la kawi , je kuna kesi nyingine ambazo shirika lako la Komesha Ufisadi linapania kufuatilia?

**18. Jeffrey**: Bila shaka. Kwa ushirikiano na jamii ya kimataifa na wafadhili, tumepata msaada wa kifedha kuendelea na uchunguzi huu. Hapana shaka haitakuwa kazi rahisi kuchunguza uovu unaoendelea nchini mwetu lakini tutajaribu kadri ya uwezo wetu.

***KW Ende***

**19. Journalist 3:** Bw. Thiongo, tunafahamu kwamba unapata ufadhili na kuungwa mkono na mataifa ya kigeni ili kuendeleza kampeni zako, Je! Raia wa nchi hii wanajukumu gani katika kupambana na ufisadi?

**20. Jeffrey:** Kwanza kabisa tunataka wote wanaohusika na kashfa hii ya nishati wajitokeze hadharani. Tunahitaji mashahidi wa kutosha ili kesi hii iweze kusonga mbele na kuwashtaki watuhumiwa.

**21. Journalist 1:** Kwanini hutaki kugombea ubunge Bw. Thiongo? **(laughs, cheers, shouts of approval)**

**22. Jeffrey:** Oh, sidhani kama nimekomaa kisiasa kufikia kiwango hicho. Mambo ni hatua kwa hatua..! Mkihitaji habari zaidi, Sylvia atawasaidia kupata nakala zaidi kuhusu ripoti yetu ya hivi punde. Pia, ataweza kujibu maswali yenu zaidi. Asanteni kwa kufika. **(gets up to leave room)**

**23. SFX:** **photo cameras clicking**

**End of Scene One**

**<u>Scene Two:</u>**

**24. Atmo:** **In a café**

**25. Sylvia:** Jeffrey, kwa hakika ulikuwa mwanzo mzuri. Mkutano huu na waandishi wa habari umefana sana, ama sivyo? Waandishi wengi wa habari wanatuunga mkono! Na nadhani masuala haya yatapata kuangaziwa kwa kina kwenye vyombo vya habari.

**26. Jeffrey:** Ni kweli, Sylvia - kufikia sasa mambo si mabaya! Naamini kwamba suala la ufisadi linapewa umuhimu mkubwa na vyombo vya habari, waandishi wa habari huwa wanapenda kufuatilia habari za aina hii. Isitoshe hakuna habari zinazouza gazeti kama suala la ngono na uhalifu. **(laughter)**

**27. Sylvia:** Ni kweli usemayo! **(laughter)**.

***KW begins*** Sikudhania kwamba mambo yatakuwa rahisi jinsi hii. Nimefurahi sana. Lakini bado kuna safari ndefu.

**28. Jeffrey:** Ni kweli kabisa, Sylvia. Na pia tuna azimio ambalo lazima tulitimize. Kwa hiyo lazima tuimarishe juhudi zetu. Kazi ianze sasa. **(enthusiastic)** "Komesha Ufisadi sasa!

***KW ends***

**29. Sylvia:** Na je kuhusu lile swali la mwisho,Jeffrey? **(shy)** Kugombea ubunge. Je, suala hilo unalifikiriaje ?

**30. Jeffrey:** Kwanza hoja hiyo sijui imetokea wapi? Nimeshangaa sana. Maana si jambo ambalo nimekuwa nikilifikiria hata kidogo. Unajua, maishani, mwanadamu hapasi kukata tamaa.…Tuna kibarua kikubwa mbele yetu hasa tangu tuanzishe shirika hili letu. Lazima tudumishe msimamo wetu Sylvia!

**End of Scene Two**

**31. Narrator:** Kwa bahati nzuri,Jeffrey amepata kuungwa mkono na vyombo vya habari katika juhudi zake za kufichua visa vya ufisadi na kuwataja wanaohusika katika kashfa hizi. Mara nyingi suala hili huwa tatizo kubwa. Hasa pale inapotokea kwamba vyombo vya habari vinasimamiwa na serikali, waandishi wengi wa habari huogopa kutekeleza kazi zao ipasavyo, katika kufichua maovu miongoni mwa jamii. Hii ni kwasababu wana hofu ya kupoteza kazi yao baada ya kuandika habari zinazoishambulia serikali. Hebu sasa tumgeukie Isaac kusikia ni yapi yanayoendelea. Isaac ni mwanafunzi katika chuo cha wanasheria na pia hufanya kazi ya muda katika kampuni moja ya uwakili.

**<u>Scene Three:</u>**

**32. Atmo:** **Office noises**

**33. Isaac:** Peter, hizi hapa stakabadhi zangu. Lazima tuzipitie kabla ya kuziwasilisha kwa mkubwa.Tunahitaji mwanasheria mwenye ujuzi aliyekomaa na mzoefu wa muda usiopungua miaka 10 mbali na vyeti vyake vya masomo.... Hayo kwanza kabla ya kuzingatia mambo mengine. Ndio maagizo kutoka kwa mkubwa.

**34. Peter:** Sawa, Isaac. Hilo linaeleweka.

**35. Isaac:** Hili bunda lote la stakabadhi hapa.… **(he picks up a pile of papers)**:

**36. SFX:** **Picking up a pile of papers**

**37. Isaac:** …ni watu waliotuma maombi na kufaulu katika mchujo wa kwanza. Sasa tutazipitia stakabadhi zao muda usiokuwa mrefu, na kisha kuwachagua watu 20 tu watakaoitwa kwa duru ya pili ya mahojiano.

**38. SFX:** **Rustles papers**

**39. Isaac:** Na hili bunda ni ...(**rustles papers)** ni.... wale ambao hawakufaulu na tunapaswa kuwatumia barua kuwaarifu kwamba maombi yao yamekataliwa..!

***KW begins***

**40. Peter:** Sawa.

**41. Isaac:** **(shouting to neighbouring office)** Mary, leo mchana utakuwa na kazi nyingi ya kuchapisha barua za watu waliotuma maombi ya kutafuta nafasi za kazi hapa kwetu. Nitakuletea barua hizo sasa hizi...!

***KW ends***

**42. SFX** **Rustling of paper**

**43. Isaac:** **(annoyed, shouting at Peter)**, Peter, unafanya nini?

**44. Peter:** Taratibu, Isaac! Napitia tu bunda hili la maombi yaliyokataliwa. Naona ni vyema pia kuwaita kwa mahojiano baadhi ya hawa ambao maombi yao yamekataliwa.

**45. Isaac:** Lakini hawana hata chembe ya ujuzi unaohitajika kwa kazi hii! Hebu tazama - **(picking up a paper)** - Mfano mzuri ni huyu bwana hapa. Alihitimu miaka minne iliyopita. Na hizi stakabadhi unazoshikilia mkononi, zinajaa kasoro nyingi tu. Haziambatani na barua yake ya maombi. Ndio maana zikakataliwa.

**47. Pe ter:** Samahani Isaac, sikubaliani na wewe. Hawa ni baadhi ya watu wenye uwezo wa kutahiniwa kwa kazi hii.

**48. Isaac:** Eti nini? Una uhakika ya unayoyasema? Kwa nini tuwaite? **(Wondering)**

**49. Peter:** Ohh , sikiliza hapa Isaac…Lazima ufahamu dunia inavyokwenda! Hawa ni jamaa zangu eti! Kama siwezi kuwapa kazi, wataweza kunisaidia kweli wakati nitakapokuwa na shida ya kutatafuta kazi wakati mwengine. Hivi ndivyo mambo yanavyokwenda. Isaac! Na mimi hivi ndivyo nilivyopata kazi hii. ‘Ukinisugua mgongo pia wewe nitausugua wako’.

**50. Isaac:** Lakini hiyo ni kinyume kabisa na utaratibu wa kuwaajiri watu wanaostahili kwa kazi... Huo ni ufisadi!

**51. Peter:** Kwani wewe ulipata vipi kazi hii? Kulingana na uwezo wako! Yaani kwa kutumia tu vyeti vya masomo, ...? Mmmm…Siamini.

**52. Isaac:** Nilifaulu katika mitihani yangu! Na … kisha rafiki ya babangu akanishauri mahala pa kutuma maombi ya kazi. Hilo tu..,.na si eti alinisadia zaidi ya hapo.

**53. Peter:** Siamini, Isaac. Wewe uliajiriwa kupitia njia ile ile ambayo inatumiwa kuwaajiri hawa wengine. Yote yategemea hadhi yako katika jamii na pia kujuana. Na sioni mtindo huu ukibadilika hivi karibuni!

**End of Scene Three**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**54. NARRATOR:** Kama tulivyosikia ni kutokana na kasumba hii ambapo ufisadi unazidi kukithiri. Isaac amekuwa mchanga kwenye kitumbua cha ufisadi. Je, ataweza kudumisha msimamo na maadili yake katika kupinga ufisadi? Je, anaamini kwamba vita dhidi ya ufisadi vitafaulu miongoni mwa jamii?

Na hadi hapo ndipo tunapofika mwisho wa makala haya, sehemu ya tano kwenye mfululizo wa mchezo huu, kusuhu suala la ufisadi kwa jina "**Tembo nyumbani**" Mchezo unaosimulia maisha halisi katika ulimwengu wa sasa.

Katika kipindi kitakachofuata, tutasikia yatakayojiri wakati Lydia Odhiambo anapomkabili mwalimu wake kuhusiana na alama alizopata shuleni huku wasichana wawili kutoka familia hiyo ya Odhiambo wakiwasilisha kesi hii katika shirika la Jeffrey "**Komesha Ufisadi sasa**". Endapo ungetaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbe. Na pia unaweza kutuma maoni yako kupitia Facebook. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!